Growing up 2030 in a digital world
GOVERNING HEALTH FUTURES
THE LANCET & FINANCIAL TIMES COMMISSION

# Kusimamia Hatima za Afya 2030:

## Matokeo muhimu na mapendekezo ya *Lancet* na Tume ya Financial Times

**Ripoti ya Tume, iliyochapishwa Oktoba 2021, inahimiza kufikiri upya mfikio katika mabadiliko ya kidijitali ya afya.**

Teknolojia za kidijitali na data zinabadilisha mifikio kwa afya na mpangilio wa mifumo ya afya, lakini mifumo ya utawala haijabadilika kwa njia ile ile. Hili limefanyiza matokeo yasiyo sawa ulimwenguni pote, kutishia demokrasia, kudhibiti mashirika ya wagonjwa na jamii, na kushusha imani na haki za kibinadamu.

Katika mwaka wa 2019, ***Lancet*** na Tume ya Financial Times kuhusu Kudhibiti hatima za afya 2030: Kukua katika ulimwengu wa kidijitali kulianzishwa ili kuchunguza jinsi ya kutumia kikamili zaidi faida na kupunguza hatari za mabadiliko ya kidijitali ili kufanyiza hatima bora zaidi za afya, hasa kwa watoto na vijana ambao watarithi namna za usimamizi zilizobuniwa leo.

Wanatume kumi na tisa kutoka sekta na taaluma mbalimbali waliletwa pamoja ili kufanyiza ripoti. Walichunguza mifikio mbalimbali ya usimamizi, miongozo ya kimaadili, na wajibu wa taasisi ambazo lazima zizingatiwe ili kuboresha afya na ustawi katika ulimwengu unaozidi kuwa wa kidijitali. Tume ilifanya kazi kwa ukaribu na Washirika ili kutegemeza mazungumzo yanayojumuisha washika dau muhimu, pamoja na vijana na kujadiliana na sekta ya kibinafsi kupitia mikutano iliyopangwa na Financial Times.

Ripoti ya Tume, iliyochapishwa Oktoba 2021, inahimiza kufikiri upya mfikio katika mabadiliko ya kidijitali ya afya.

**Inategemezwa na:** CHILDREN'S INVESTMENT FUND FOUNDATION · fondation BOTNAR · wellcome · Swiss Agency for Development and Cooperation SDC

# MATOKEO MUHIMU

### Mfumo wa kazi unaotegemea thamani wa kudhibiti hatima za afya

Nchi nyingi bado hazijaanza kutumia mfikio unaotegemea mshikamano wa data, imani ya kidijitali, haki za kibinadamu, uwajibikaji, na kushiriki kwa umma. Mambo haya ndiyo muhimu kwa kuendeleza afya kwa wote, kupunguza ukosefu wa usawa na kutatua mahangiko ya faragha.

### Kuzungumzia viukilia vya afya ya kidijitali

Mfikio wa ushikamano kwa data ya afya na kuzungumzia viukilia vya afya ya kidijitali ni muhimu ili kutumia kikamili thamani ya afya ya umma ya mabadiliko ya kidijitali. Hata hivyo mambo haya yanakosekana katika mifikio mingi ya utawala.

### Kuwaweka vijana katikati

Vijana wanachangamshwa kuhusu jinsi faida za mabadiliko ya kidijitali zitakavyoathiri afya na hali yao njema na wanahangaikia hatari. Mtazamo na mahitaji ya vijana mara nyingi hayatangulizwi kabisa katika utengenezaji wa sera au ustawishaji wa teknolojia.

# MAPENDEKEZO KWA UTENDAJI

1. Zungumzia jukumu la teknolojia za kidijitali kama viukilia vya afya
2. Jenga muundo wa utawala unaochochea imani
3. Dhibiti data ya afya ili kuongeza thamani yake ya umma
4. Wekeza katika wawezeshaji wa mabadiliko ya kiteknolojia kwa ajili ya afya ya umma

Soma ripoti kamili kwenye tovuti yetu
www.governinghealthfutures2030.org